(Cover page)

**E K L E S I A   Y A   M I T U M E**
**(The Apostolic Ecclesia)**

# KIRI LA IMANI

*Ila neno hili naungama kwako ya kwamba, Kwa njia ile ambayo waiita uzushi, ndivyo Nilivyo Mwabudu Mungu wa baba zetu, Nikiyaamini yote yanayopatana na torati na yaliyoandikwa katika vyuo vya manabii:*

*Paulo - Matendo ya Mitume*

*Hawa wote wakafa katika imani, wasijazipokea zile ahadi, bali wakiziona tokea mbali na kuzishangilia, na kukiri kwamba walikuwa wageni, na wasafiri juu ya nchi.*

*Waraka wa Waebrania*

*Nakuagiza mbele za Mungu anayevihifadhi hai vitu vyote, na mbele za Kristo Yesu, aliyeyaungama maungamo mazuri yale mbele ya Pontio Pilato. Kwamba uilinde amri hii pasipo mawaa, pasipo lawama, hata kufunuliwa kwake bwana wetu Yesu Kristo.*

*Paulo kwa Timotheo*

*Kila roho lkiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu. Na kila roho isiyokiri kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili haitokani na Mungu.*

*Waraka wa kwanza wa Yohana.*

**E K L E S I A   Y A   M I T U M E**
**(The Apostolic Ecclesia)**

# KIRI LA IMANI

*(Sahihisho la maelezo ya imani ya awali)*

*Ila neno hili naungama kwako ya kwamba, Kwa njia ile ambayo waiita uzushi, ndivyo nilivyo Mwabudu Mungu wa baba zetu, Nikiyaamini yote yanayopatana na torati na yaliyoandikwa katika vyvo vya manabii.*

*Paulo - Matendo ya Mitume*

*Hawa wote wakafa katika imani, wasijazipokea zile ahadi, bali wakiziona tokea mbali na kuzishangilia, na kukiri kwamba walikuwa wageni, na wasafiri juu ya nchi.*

*Waraka Kwa Waebrania*

*Nakuagiza Mbele za Mungu anayevihifadhi hai vitu vyote, na Mbele za Kristo Yesu, aliyeyaungama maungamo mazuri yale mbele ya Pontio Pilato. Kwamba uilinde amri hii pasipo mawaa, pasipo lawama, hata kufunuliwa kwake bwana wetu Yesu Kristo.*

*Paulo kwa Timotheo*

*Kila roho lkiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu. Na kila roho isiyokiri kwamba Yesu Kristo amekuja katika Mwili haitokani na Mungu.*

*Waraka wa Kwanza wa Yohana*

# K I R I   L A   I M A N I

*(Oktoba 2004)*

## DIBAJI

**"Kila akiriye ya kuwa Yesu ni mwana wa Mungu, Mungu hukaa ndani yake, naye ndani ya Mungu."**

**Waraka wa kwanza wa Yohana 4:15**

Neno "Kiri" katika Utaratibu ulio idhinishwa na bibilia linatafsiriwa kutokana na kiyunani 'homologeo' ombala linamaanisha "kunena kitu kimoja kama kingine". Katika kushughulikia magumu ambayo yalitokea kwenye Eklesia (Jumuia ya waumini) katika Wakorintho, Mtume Paulo alisihi kuwepo na umuhimu wa waumini wote kunena kitu kimoja, ili kusiwe na migawanyiko, bali wote waunganike kikamilifu pamoja katika wazo moja na hukumu moja, kilichozingatiwa kama mwenendo wa umuhimu wa Eklesia kama mwili mmoja wa Kristo katika karne ya kwanza, kinabaki vile hata katika karne ya ishirini na moja.

Lengo la "Kiri la imani" ni kuweka bayana kwa utaratibu, kama ilani ya wazi, vitu ambavyo kwa uhakika vinaaminiwa na wafuasi wote wa Eklesia. Kwa kufupisha mafundisho ya Bibilia katika lugha rahisi ya kueleweka, kwa kuegemezwa na marejeleo muhimu ya mateuzi, namna inatolewa ya kudhihirisha ulinganifu wa itikadi ambayo mitume walitamani.

Kiri ni jumla ya uonyesho wa imani, kutilia mkazo utayari kwa upande wa waumini kueleza wazi kile ambacho wanaamini bibilia yafunza, katika vitengo kadhaa vyenye umuhimu. Haya yanaeleza nafsi ya mwili mmoja wa Kristo kinyume na majina mengi na madhehebu ya "UKristo" katika ulimwengu wa kisasa.

Kunao wengi ambao watadhibitisha kuamini kwao kwenye bibilia kwa namna ya kawaida, lakini katika tathmini hupatikana kuwa kinyume na mafundisho yake, wanapoulizwa kueleza jinsi wanavyoelewa hoja fulani za mafundisho. Ingawa huonyesha heshima ya juujuu kwa vigezo fulani vya maandiko, wao huepuka ridhaa azimu ya sehemu zingine muhimu za neno lenye pumzi ya Mungu.

Hili kiri linawekwa bayana katikia kigezo chema (Mafundisho ya kukubaliwa) na kigezo chenye dosari (Mafundisho ya kukataliwa), ili kuhakikisha kuwa hakuna kosa katika msimamo wa Eklesia kwa hoja fulani, mtu anaweza toa idhini kwa funzo mahsusi katika hali ya uzuri wake, lakini pia kwa wakati ule awe mnyamavu kukubali kano la mawazo mengine ambayo hii idhini inadokeza. "Kila shauri la kuyakinisha lina kinyume, kila ndio ina la: na ikiwa mtu hayuko tayari kukubali ile 'la', basi inaonyesha hata 'ndio' yake haina umuhimu mkubwa."

Kiri ni Masaada tayari kwa waumini kama njia ya kuadilisha, huku muhtasari wa sheria ya Kristo ukitoa kumbusho dhabiti la mwenendo ambao ni "Bora kwa kazi ambayo wameitwa, kwa ajili yake", kama vile inavyodokezwa katika dibaji ya toleo la kwanza (Ukurasa wa 26), sheria au kanuni ya kutii inafaa kupatikana katika sheria ya Kristo, Inatamatika katika huu usemi wake – "Ikiwa mtazishika amri zangu, mtadumu katika upendo wangu."

Kiri itathibitisha kuwa yenye huduma katika kushuhudia na pia katika kukanusha, ili jibu katika kuitetea injili lipewe kwa kila mmoja anayeuliza, kwa njia ya kuthibitisha kupitia maandiko, waumini wanaweza kuwa tayari kutoa sababu kwa ajili ya tumaini lililo ndani yao. Kiri pia itathibitisha kuwa ya muhimu kama mwongozo kwa wadadisi wenye kichocheo na kutoa namna ya kutafuta katika maandiko ikiwa vitu hivi viko hivyo.

Hili kiri, ingawa ni sahihisho, limesimamishwa katika kazi ya awali ya wandugu waliojithamini kwa ajili ya kazi zao. Ingawa kwa muda wa miaka mingi, ukweli wa Bibilia umepingwa kutoka kwa maadui wanaoinuka ndani na nje, kwa hivyo imefikiriwa kuwa ya manufaa kutoa msimamo wa maandiko juu ya hoja zile zinazojitokeza.

Maelezo ya imani yamechukuliwa na baadhi ya watu kama yasiyobadilishwa kana kwamba yameandikwa kwa mawe. Hili limepelekea kuafikia mwisho kuwa ikiwa ubishi utatokea ambao haujaangaziwa na maelezo, basi hauwezi kuwa hoja muhimu ambayo yaweza kuathiri ushirika. Hili halifai kuwa hivyo, maelezo hayo ni kazi zinazokubaliwa za wanadamu na hayafai kuinuliwa zaidi ya viwango vyake halisi kuinuliwa za wanadamu na hayafai kuinuliwa zaidi ya viwango vyake halisi. Sahihisho ni lazima ili kuangazia hoja zile zile ambazo zinapinga maandiko na zinaweza kudhoofisha uamuzi wa waumini kushikilia kilicho chema. Ijapokuwa umakini umepewe shughuli ile, madai ya uhakika na sheria yameachiwa wengine kufanya. Kunayo

sheria moja tu isiyo na dosari katika maswala ya imani na mwenendo, nayo ni maandiko matakatifu yenyewe.

Hili kiri linajaribu kutoa kanuni sahihi ambayo "Inajaribu Roho" ili kupima madai yenye ubishi ya mafundisho mengi ya uongo ambayo yamejaa katika nyakati za kisasa za Mataifa; na maandiko yanayofaa; kama njia ya kunyamazisha upumbavu wa watu wajinga.

Usiaibike juu ya imani yako, ni kwa sababu ya hii injili ambayo mitume walihatarisha maisha yao kwa ajili ya Bwana Yesu na watakatifu wamedhulumiwa, wakiumia kwa kupoteza vitu vyote. Walakini Ikiwa Eklesia Itabaki kuwa ya kweli kwa mwito wake, malango ya kuzimu hayataishinda.

Mwisho, kiri linafupisha lakini haliwi mbadala wa maandiko matakatifu ambayo kila mara na kwa vitengo vyote yanabaki kuwa yenye manufaa zaidi.

**"Na waende kwa sheria na ushuhuda; Ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi." Isaya 8:20**

**“Hamjui ya kuwa kwake yeye ambayo mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki. Lakini Mungu ashukuriwe kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mlitii kwa mioyo yenu ile**

# NAMNA YA ELIMU

**Ambayo mliwekwa chini yake, na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa, wa haki.”**

**Paulo - Warumi 6:16-18**

# E K L E S I A   Y A   M I T U M E
**(The Apostolic Ecclesia)**

Jumuia ya waumini katika ahadi zilizo kwenye maagano ya Mungu kwa Ibrahimu na Daudi, kama zilivyowasiliswa katika mafundisho ya Bwana Yesu Kristo na Mitume wake kuhusu "Ufalme wa Mungu na jina lake Yesu Kristo," ambao wamebatiza kwa jina la baba na la mwana na la Roho Mtakatifu.

Lengo la hii Jumuia ni kuendeleza Imani iliyo pokewa na mitume kutoka kwa Bwana Yesu Kristo (Inayofupishwa katika kiri lifuatalo) na utekelezaji wake baada ya mifano ya wale walioagizwa na mitume kwa:

Kumkumbuka Bwana Yesu Kristo, katika siku ya kwanza ya Juma, kwa namna iliyoanzishwa na yeye kwa kuumega mkate na kunywa divai pamoja, kutangaza mauti ya Bwana hadi kuja kwake.

Kusherehekea sifa kuu za Mungu na kutoa dua, maombi, mateteo na kutoa shukrani.

Kusoma, kuchunguza na kufasiri maandiko matakatifu ili kutoa mwelekeo wa unyofu, muongozo mwafaka, ushauri na kufariji.

Kuimarisha na kuitangaza injili ya Ufalme na utetezi wa kweli ya Bibilia kinyume na ufisadi wa kidini wa nyakati hizi.

Ushirika wa watakatifu na msaada mwafaka wakati wa uhitaji.

Kudumisha umoja wa roho kwenye fungo la amani katika mwili mmoja, kwa wote kujitahidi pamoja kushika na kuhifadhi mafundisho ya Bwana Yesu Kristo.

Tunatambua Kama Ndugu wa Kristo wote ambao wamebatizwa baada ya kuyakubali mafundisho na maagizo ya Kristo na Mitume wake (kwa kulishika hili kiri) na wanaojitahidi kuzishika amri za Bwana na Mwokozi, Yesu Kristo kwa Mtazamo wa kuwafanya watu wawe tayari kwa ajili ya Bwana, atakapoonekana.

Maswali yote yanakaribishwa na yanaweza kuelekezwa kwa:

The Apostolic Ecclesia
PO Box 468
Bungoma
Kenya
(50200)

Email: bibletruthkenya@gmail.com

Further Contact Details:

| |
|---|
| |
| |
| |
| |
| |
| |

UK Contact:

Local Secretary
The Apostolic Ecclesia
3 Norman Road
Dartford
DA1 1LE
United Kingdom

Email: bibletruth@btinternet.com

Website: www.bible-truth.co.uk

# K I R I  L A  I M A N I

**(Confession of Faith)**

**Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.** Warumi 10:10

## M S I N G I

Tunaamini kuwa kitabu kinachojulikana kama Bibilia ni neno la Mungu na kina chimbuko pekee la ufahamu kuhusu Mungu na malengo yake yanayopatikana duniani kwa wakati wa sasa. Haya maandiko matakatifu yaliyo na agano la kale na agano Jipya, yakijumuisha maandiko ya musa, manabii, Saburi na Mitume wake Bwana Yesu Kristo, kwa ujumla yalipewa kwa pumzi ya Mungu kupitia kwa waandishi, na kwa hivyo hayana makosa katika sehemu zote, isipokuwa dosari zinaweza kuwapo kutokana na makosa ya kunakili na kutafsiri. Kuamini katika haya maandiko matakatifu, ambayo yana habari zote za lazima ili, kuupokea wokovu, ni kanuni muhimu ya kuwa katika ushirika na Mungu na Bwana Yesu Kristo.

Luka 24:44; 2 Timotheo 3:16; Kumbukumbu 29:29; Matendo 7:38; 3:18,21; 8:35; 10:43; 26:22; 13:26,27; 24:14; 1 WaWakorintho 2:13; Waebraniarania 1:1; 2 Petro 1:21; 1 Wakorintho 14:37; Mithali 30:5-6; Isaya 55:11, Nehemia 9:30; Yohana 10:35; 2 Petro 1: 3-4; Warumi 3:2.

## UKWELI WA KUPOKEWA

Mafundisho ya Bibilia yote ambayo yafuatayo ni muhtasari:

1) Kuwa kuna Mungu mmoja, mwenye mamlaka, mwenye uwepo, asiye angamia, adumuye milele, mwenye nguvu, muumbaji mwenye hekima kuu na mhifadhi wa mbingu na dunia na vitu vyote, chanzo cha uzima, aishiye kwenye nuru isiyokaribiwa. Lakini aliye kila mahali katika Roho wake, ambayo kwake tunaishi na kutembea na kuwa na nafsi zetu.

Mariko 12:29-32; Matendo 14:15;17:24-29; 1 Wakorintho 8:4-6; Waefeso 4:6; I Timotheo 1:17; 2:5; 6:15-16; Isaya 40:13-26; 43:10-12; 44:6-8; 45:5-8,12; 46:9-10; 55:8-9; Ayubu 38-40; Kumbukumbo 6:1-4; Nehemia 9:6; Ayubu 26:13; Saburi 24:8; 146:6; 148:5; Yeremia 10:12-13; 27:5; 32:17-

19; 51:15; 1 Nyakati 29:11-13; Saburi 62:11; 145:3; Isaya 26:4; Ayubu 9:4; 36:5; Saburi 92:5; 104:24; 147:4-5; Warumi 16:27; 1Timotheo 1:17; 2 Nyakati 16:9; Ayubu 28:24; 34:21; Saburi 33:13-14; 44:21; 94:9; 139:7-12; Mithali 15:3; Yeremia 23:24; 32:19; Amosi 9:2-3; Saburi 123:1; 1 Wafalme 8:30-39; 43, 49; Matayo 6:9.

2) Kuwa huyu Mungu pekee wa kweli, ambaye njia na mawazo yake yanazidi yetu, alifunuliwa kwa Ibrahimu, Isaka na Yakobo, kwa namna ya kimalaika kuwatembelea na katika maono: Alijifunua kwa musa katika kichaka kilichokuwa kinachomeka (lakini hakiungui) na katika Sinai alipofanya jina lake lijulikane, Yahwe; Pia alijidhihirisha katika Bwana Yesu Kristo.

Yohana 17:3; Isaya 55:8-9, Waebraniarania 1:7; Mwanzo 12:7; 17:1; 18:1; 26:2; 28:12-15; Kutoka 3:2-22; 19:17-25; Waebraniarania 1:1-2; Yohana 1:14; 17:6; Luka 10-22; Matendo 2:22,23; 1 Yohana 1:1-3.

3) Kuwa Yesu wa Nazareti ni Mwana wa Mungu, aliyezaliwa katika bikira maria, pasipohusisha mwanamme, kupitia kwa uwezo wa Roho Mtakatifu kuwa huyu Yesu katika siku zake za mwili alikowa mtu apatikanaye na kufa, aliyezaliwa na Mungu ili awe Mtumishi wake wa kipekee, kama llivyothibitika baadaye katika kutawazwa na Roho Mtakatifu aliyeshuka kwake katika ubatizo wake kwenye mto Yordani, alipobatizwa na Yohana Mbatizaji. Kwa hivyo alikowa "Emmanueli" linalomaanisha "Mungu Pamuja nasi", Masihi aliyeahidiwa, Mungu kudhihirika katika mwili.

Marko 1:1 9-11; Matayo 1:23; 1 Timotheo 3:16; Matendo 2:22-24, 36; 3:26; 8:37; 10:38; Matayo 1:18-25; Luka 1:26-35; Wagalatia 4:4; Isaya 7:14; Matayo 3:16-17; Isaya 11:2; 42:1; 61:1; Waebraniarania 5:7; 2:14; Yohana 3:34; 7:16; 8:26-28; 14:10-24.

4) Kuwa kunayo Roho moja tu ya Mungu, ambayo ni nguvu za Mungu zinazoenea kutoka kwake, zikijaza nafasi zote na kujumuisha umoja na nafsi yake mbinguni. Kwa hii nguvu isiyo na asili, anaumba na kuhifadhi vitu vyote, na Kwa hii nguvu isiyo na asili, anaumba na kuhifadhi vito vyote, na kwa hii nguvu alinena kupitia kwa manabii na mitume na akajidhihirisha katika Mwana. Kupitia kwa huu uwezo, watumishi wake wametenda miujiza. Inapotengwa kwa kazi ya kipekee au lengo fulani, hii nguvu huitwa Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu haijatolewa katika kizazi cha sasa kama ilivyokuwa katika kizazi cha Mitume lakini neno lake lililozungumzwa kupitia kwa

manabii na mitume lina nguvu ya kuelimisha na kutakasa na linafaa kwa wokovu, si lazima kutolewa kwa Roho Mtakatifu ndipo yeyote aamini ushuhuda wake ulioandikwa.

Mwanzo 1:2; Saburi 139:7-12; Ayubu 26:13; Luka 1:35; 2 Petro 1:21; 2 Timotheo 3:16; Matendo 11:16-17; 1 WaWakorintho 13:8-10; 2 Petro 1:2-4; Matendo 8:12, 15-16.

5) Kuwa kuonekana kwa Yesu wa Nazareti katika dunia kulilazimishwa na nafasi na hali ambayo wanadamu walikuwa wameingia, kwa kadhia zilizofungamana na mtu wa kwanza.

1 WaWakorintho 15:21-22; Mwanzo 2:17; Warumi 5:12-19; Mwanzo 3:15-19; Yohana 1:29; 3:16; 2 WaWakorintho 5:19-21; 1 Yohana 4:14; Mwanzo 1:31; 1 Timotheo 1:15.

6) Kuwa mtu wa kwanza Adamu aliumbwa na Mungu kutoka kwenye mavumbi ya ardhi, kama roho inayoishi au mwili asili wa uhai “mwema kabisa” kwa namna na hali. Aliwekwa chini ya sheria ambayo kuendelea kwa uhai kulitegemea utiifu.

Mwanzo 2:7; 18:27; Ayubu 4:19; 33:6; 1 WaWakorintho 15:46-49; Mwanzo 2:17.

7) Kuwa Adamu aliivunja hii sheria, na kwa hesabu ya hii dhambi alihukumiwa kurudi kwa ardhi ambayo alitwaliwa, hukumu iliyonajisi na kuwa sheria ya asili ya nafsi yake na kupishwa kwa wazao wake wote.

Mwanzo 3:15-19; 22-23; Saburi 90:3; 1 Petro 1:24; 2 WaWakorintho 1:9: Warumi 7:24; 2 WaWakorintho 5:2-4; Warumi 7:18-24; Wagalatia 5:16-17; Warumi 6:12, Yohana 3:6; Warumi 5:12, 1 WaWakorintho 15:22, Saburi 51:5; Ayubu 14:4.

8) Kuwa mtu kama mzaliwa wa Adamu ni kiumbe kipatikacho na kufa, ambacho hukoma kuwepo kifo kinapotekea, na katika mauti hakuna uhai, au mawazo au dhamiri.

Mhubiri 9:5,6,10; Saburi 6:5; 39:5,12-13; 115:17; 146:3-4; Isaya 38:18-19.

9) Kuwa dhambi ni uvunjaji wa sheria takatifu “Ibilisi” (Anenwaye na Paulo katika Waebraniarania 2:14 kuwa na nguvu ya mauti) ni dhambi katika namna zake kadhaa inayodhihirika miongoni mwa watu. Inadhihirika kibinafsi katika namna yetu ya kiasili, na kwa ujumla katika siasa za kibinadamu na mashirika ya kidini

Ikiwakilishwa kwa maelezo ya maandiko kama “Nyoka”, “Mzao wa nyoka”, “Joka”, “Yule Mwovu”, “ulimwengu”, “Ibilisi na Malaika wake”, Neno shetani linamaanisha “Mpinzani” na linatumika kwa wanadamu, kibinafsi na kiujumla, wenye uadui na Mungu. Hakuna kitu kama kiumbe kikuu kiitwacho Ibilisi.

1 Yohana 3:4; Waebraniarania 2:14; Warumi 5:12; 7:17,23; Yakobo 1:13-15; Ufunuo 12:9; 20:2; Yakobo 4.4.

10) Kuwa Mungu katika upendo na Rehema zake alifanya mpango wa kurudisha, pasipo kuweka kando sheria yake iliyo kamili na ya lazima juu ya dhambi na mauti, Ili mwishowe aokoe jamii kutokana na angamio na kuijaza dunia na watu wasio na dhambi wenye kuishi milele.

Yohana 3:16, Warumi 5:8; Waefeso 3:9-11; Hesabu 14:21; Habakuki 2:14; Ufunuo 21:4; 2 Timotheo 1:10; 1 Yohana 2:25; 2 Timotheo 1:1; Tito 1:2; Warumi 3:26; Yohana 1:29.

11) Kuwa Mungu alianzisha huu Mpango kwa kutoa ahadi kwa Adamu, Ibrahimu na Daudi, akifafanua baadaye kinaganaga kwa namna kuu kupitia kwa huduma ya manabii.

Mwanzo 3:15; 22:18; Saburi 89:34-37; Isaya 45:23; Wafilipi 2:10; Hosea 13:14; Isaya 25:7-9; 51:1-8; Yeremia 23:5.

12) Kuwa huu Mpango wa upatanisho ulitazamiwa katika mwana wake, Yesu Kristo ambaye, kama mzao wa mwanamke ilivyoahidiwa, ilikuwa adhihirishwe ili kukiponda kichwa cha nyoka, kuharibu chanzo cha dhambi na madhara yake yote. Katika kuonekana kwake Mara ya kwanza, Yesu aliharibu nguvu za dhambi juu ya mwili wake, na katika kuonekana kwake mara ya pili, ataharibu nguvu za dhambi juu ya wale watakaokuwa na kibali mbele ya kiti chake cha hukumu. Mwisho wake, ataharibu dhambi miongoni mwa jamii za wanadamu, ambapo mwishowe dhambi itaondolewa kabisa duniani.

Wakolosai 1:19, 20; 2 WaWakorintho 5:18,19; Mwanzo 3:15; Warumi 8:3;1 Yohana 3:5; Waebraniarania 2:14,15; 1 WaWakorintho 15:22-25; Ufunuo 21:4.

13) Kuwa Yesu Kristo, Katika kutimiza ahadi za Mungu, alizaliwa na nyama na damu kutokana na Mwanamke jinsi ilivyokuwa asili, katika utaratibu wa Ibrahimu na Daudi, chini ya Torati ya Musa. Alimiliki asili yao ya Kibinadamu iliyo chini ya laana kutokana na kosa la

Adamu. Kwa hivyo alishiriki Mateso kutokana na Madhara yaliyoletwa na mwili huu. Mtu wa huzuni aliyeyafahamu Masikitiko, Pamoja na kifo kilichowapata wanadamu wote. Akiwa na tamaa kama zetu, alijaribiwa kwa namna zote jinsi tunavyoja ribiwa, ingawa hakutenda dhambi yoyote. Kama Mwana wa Mungu, katika kuzaliwa kwa utakatifu na kupewa Roho Mtakatifu, alikuwa Munga aliyedhihirika katika mwili. Katika Maisha yake ya kutii kikamilifu sheria takatifu, ambayo kwake. Mungu aliilaani dhambi katika mwili, yeye alikuwa neno lililofanyika mwili.

1 Wakorintho 15:45; Waebrania 2:14-16; Warumi 1:3; Waebrania1:9; 5:8-9; Warumi 5:19-21; Wagalatia 4:4-5; Warumi 8:3-4; Waebrania 2:15; 9:26; Wagalatia 1:4; Waebrania 7:27; 5:3-7; 2:17; Isaya 53:3; Warumi 6:10; 6:9; Matendo 13:34-37; Ufunuo 1:18; Yohana 5:21-22; 26-27;14:3; Ufunuo 2:7; 3:21; Matayo 25:21; Waebrania 5:9; Mariko 16:16; Matendo 13:38-39; Warumi 3:22; (Saburi 2:6-9, Danieli 7:13-14; Ufunuo 11:15; Yeremia 23:5; Zekaria 14:9; Waefeso 1:9-10) [Hivi vifungu sita vinafaa kuchunguzwa kwa pamoja.]

14) Kuwa ilikowa huduma ya Yesu Kristo kutangaza habari njema kwa jamaa yake, Wayahudi, na kuwa huu ujumbe, ulioshuhudiwa na Mungu kupitia kwa kazi kuu na ishara, ulikuwa ni mwito wa toba kutoka kila tendo la uovu, kuthibitisha kuwa Mwana Mtakatifu na mfalme wa Wayahudi, kutangazwa kwa urejesho wa Ufalme wa Wayahudi kupitia kwake na kuwa angetimiza mambo yote yaliyoandikwa katika sheria na Manabii kumhusu yeye Mwenyewe kwa utukufu wa Mungu na Manufaa yao ya milele.

Mariko 1:15; Matendo 2:22; Matayo 4:17; 5:20-48; Yohana 10:36; 9:35; 11:27; 19:21;1:49; Warumi 15:8; Matayo 27:11-43; Yohana 10:24-25; Matayo 19:28; 21:42-43; 23:38-39; 25:14-46; Luka 4:43; 13:27-30: 19:11-27; 22:28-30; Matayo 5:17; Luka 24:44.

15) Kwa kukabidhi huu ujumbe, alikamatwa na kuawa na Wayahudi na Warumi. Hawa walikuwa vyombo tu katika Mkono wa Mungu, ili kutimiza yale ambayo yalikuwa yamepagwa na kujulikana na Munga ili yatokee baadaye. Hili lilikuwa kuhukumu dhambi katika mwili Kupitia kuutoa mwili wa Yesu Mara moja kwa ajili ya wote, kama dhabihu kutangaza utukufu wa Mungu, kama msingi wa msamaha wa dhami. Katika mateso yake, alichukua majonzi na huzuni za wengine; alitiwa jeraha kwa ajili ya maovu yetu, alichubuliwa kwa ajili ya udhalime wetu, na kwa mapigo yake sisi tumepona. Yalikuwa ni

mapenzi ya Mungu kumtesa Yesu; Kumfanya kondoo anayepelekwa kwa kichinjio, kuwa dhabihu ya dhambi.

Luka 19:47; 20:1-26; Yohana 11:45-53; Matendo 10:38-39; 13:26-29; 4:27-28; Warumi 8:3; Waebrania 10:10; Warumi 3:25-26; Matendo 13:38; 1 Yohana 1:7; 1 Petro 3:18; 2:24; Waebraniarania 9:14; 7:27; 9:26-28; Wagalatia 1:4; 4:4-5; Waebrania 9:15; Luka 22:20; Matayo 26:28; Matendo 2:23; 3:13,18; 7:52; 26:23; Isaya 53:3,4,5,7,10,11.

16) Kuwa katika kusulibiwa kwake, dhambi ilihukumiwa kwenye mwili wa namna sawa na ule uliokosa katika Edeni; Zaidi ya hayo, kuninginizwa kwenye mti, Yesu aliwekwa chini ya laana ya sheria ya Musa ambayo hukumu yake ilikuwa kifo. Katika kifo chake, sheria ya musa ilitimiza yote ambayo ilihitaji, ili katika ufufuo wake, ile sheria. isiwe tena na dai lolote juu yake. Kristo hivyo akawa mwisho wa sheria kwa utakatifu na mzaliwa wa kwanza wa uumbaji mpya, kwa wote ambao wanafungamanishwa naye. Wote Wayahudi na Wayunani ambao wanamwendea Mungu kupitia kwa huyu aliyesulibiwa, lakini akafufuka, muwakilishi wa kutotii kwa Adamu ambaye kwake kizazi kinasamehewa. Kwa hivyo kimaumbile damu yake inatakasa dhambi.

Warumi 8:3; Wagalatia 4:4-5; 2 Wakorintho 5:21; Wagalatia 3:13; Warumi 10:4; Waefeso 1:7; Wakolosai 1:14-18; Waebrania 9:14; I Petro 1:19; 1 Yohana 1:7; Ufunuo 1:5; 5:9.

17) Kuwa wale walioishi Kabla ya kuwepo kwa Yesu Kristo kama vile Ibrahimu, Manabii na Ndugu chini ya sheria ya musa wanatakaswa na kuhesabiwa haki kupitia kwa Imani yao katika ahadi zilizotolewa kwenye maagano kati ya Mungu kwa Ibrahimu na Daudi kuhusu mzao wa ahadi. Haya maagano yaliweza kutekelezwa kwenye dhabihu ya kifo chake Yesu Kristo. Kuanzia siku ya pentekosti hadi kurudi kwake Yesu Kristo, ni wale Wayahudi na Wayunani ambao wamebatizwa baada ya kuamini zile ahadi zilizowekwa kwenye maagano na vitu kuhusu jina lake Yesu Kristo ambao wanahesabiwa haki au kuhesabiwa watakatifu. Kunaye Mungu mmoja tu ambaye atathibitisha kutahiriwa katika Imani na kutotahiriwa katika Imani, Aidha chini ya sheria au baada ya sheria, wenye haki wataishi kwa Imani, ambayo isipokuwepo haiwezakani kumpendeza Mungu.

Warumi 15:8,3:25; Waebrania 9:15; Matendo 4:10-12; Warumi 3:30; Wagalatia 3:11; Waebrania 10:38; 11:6.

18) Kuwa sheria ya musa baada ya kukamilishwa katika kifo na ufufuo wa Yesu Kristo, hakuna kipengele chake chochote ambacho kinawafunga Ndugu wa Kristo Isipokuwa walioamriwa tena na Kristo au kupitia kwa Mitume, kwa hivyo kusisitiza juu ya kuishika sabato kama inavyotakiwa na madhehebu na dini fulani haiambatani na maandiko.

Matendo 13:39; Warumi 3:20,28; Wagalatia 2:16; 3:11; 5,4; Waefeso 2:15; Wakolosai 2:14-17; Waebrania 10:14.

19) Kuwa katika siku ya tatu, Mungu alionyesha upendo wake mwema na wa rehema kwa kumfufua Yesu kutoka wafu, kwa sababu kama mtu mwenye utakatifu uliokamilika, haingewezekana yeye kuendelea kutawaliwa na mauti. Nabii Daudi aliyaona na kuuzungumzia ufufuo wa Kristo, kuwa hataachwa kuzimu, wala mwili wake kuona uharibifu. Huyu Yesu aliinuliwa juu na Mungu, akimiliki lango la adui wake mkuu mauti; kwa hili, mitume wote walikuwa mashahidi. Kisha Mungu alimpa uzima wa milele na kumuinua kama mfalme na mwokozi, kuketi katika mkono wake wa kuume mbinguni. Ufufuo wa Kristo ni hakikisho la Mungu kuwa atarudi kuutawala ulimwengu katika utakatifu. Kwa sasa, kama mfalme kwa mfano wa Melkizedeki, Yesu ndiye mpatanishi pekee kati ya Mungu na mwanadamu Katika utaratibu wa kusanya kutoka miongoni mwa wanadamu, watu wataokolewa kwa kuamini na kuitii kweli.

Matayo 16:21; 17:23; 20:19; 27:64; Mariko 9:31; 10:34; Luka 9:22; 18:33; 24:7,46; Matendo 10:40; 1 Wakorintho 15:4; 2 Samweli 7:15, Saburi 91:14; Waebrania 5:7; Luka 24:51; Waefeso 1:20; Matendo 2:31-33; 5:31; 17:31; Saburi 110:4; Waebrania 6:20; Matendo 4:12; 1 Timotheo 2:5; Waebrania 12:24; Warumi 16:26; 2 Wathesalonike 2:13.

20) Kuwa Yesu Kristo ni kuhani juu ya nyumba yake na anawaombea ndugu zake wakosaji ikiwa wataacha na kuzitubu dhambi zao. Yeye hauombei ulimwengu wala wakosaji walioachwa kwa hali ya kutotii.

1 Timotheo 2:5; Waebrania 2:17; 3:1,2,6; 4:14-16; 8:1; Matendo 15:14; 13:39; Yohana 17:9; Waebrania 10:26; 1 Yohana 2:1; 1:9; Mithali 28:13; 2 Petro 2:20-22.

21) Kuwa baada ya kufufuka, Yesu Kristo aliwatuma Mitume wake kuitangaza injili ya wokovu kupitia kwake kama jina pekee chini ya mbingu ambalo wanadamu wanaweza kuokolewa kwalo, kwanza

kwa Wayahudi, na baadaye kwa Mataifa, kutwaa miogoni mwao watu kwa ajili ya jina lake.

Matayo 28:19-20; Luka 24:46-48; Matendo 1:8; 26:16-18; 4:12; 15:14.

22) Kuwa injili au habari njema inajumuisha vitu kuhusu Ufalme wa Mungu na jina lake Yesu Kristo.

Matayo 4:23; Marko 1:14; Luka 4:43; 8:1; 9:2; Matendo 8:12; 19:8;10,20; 28:30-31.

Hivi "Vitu" ni hakika ya mambo yenye uhusiano na maandiko ya manabii na mitume kuhusu Ufalme wa Mungu ambayo yamewekwa kimuhtasari katika aya kumi na nne zifuatazo.

## KUHUSU UFALME WA MUNGU

23) Kuwa Mungu atausimamisha Ufalme duniani ambao utapindua namna zote za utawala wa wanadamu na kuufanya kuwa Ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake.

Saburi 2:8; 72:8,9; 145:10; Danieli 2:44; 7:13-14; Ufunuo 11:15; Isaya 2:3,4; 32:1,16; 11:9-10.

24) Kuwa kwa lengo hihi, Mungu atamtuma Yesu Kristo mwenyewe duniani katika mwisho wa nyakati za Mataifa, kama ilivyoandikwa katika kitabu cha ufunuo kwenye mfano wa (Page 12) Muhuri wa sita, na kujulikana kwa urejesho wa utawala wa taifa la Israeli katika makaazi yao ya jadi.

Matendo 3:20-21; Saburi 102:16,21; 2 Timotheo 4:1; Matendo 1:9,11; Danieli 7:13; Luka 21:24-27; Warumi 11:25-26; Ufunuo 16:12-16; Ezekieli 36-37.

25) Kuwa katika kuonekana kwake kwa pili, Yesu atausimamisha Ufalme wa Mungu kwa kuwarejeshea Israeli Ufalme wao, na hali kadhalika kueneza utawala wake kwa Mataifa yote ya duniu. Hili litahusisha kuondole wa kwa mifumo yote ya uongozi iliopo yenye uovu na pia miungano ya madhehebu.

Warumi 2:10; Matendo 1:6; Isaya 49:6; 59:20; 60:1-5; Ezekieli 36:24-36; Zekaria 12:7; Hesabu 14:21.

26) Kuwa urejesho wa Ufalme kwa Israeli utahusisha kuwasanya wote waliochaguliwa na Mungu ijapokuwa wametawanyika katika Mataifa, Wayahudi; Kurudishwa kwenye nchi ya baba zao, sehemu waliokowa wakimiliki awali, baada ya kutwaliwa Kutoka “Ukiwa wa vizazi vingi”; iitwayo nchi yote ya Kanaani, aliyoahidiwa Ibrahimu na mzao wake, ambaye ni Kristo, kupitia kwa agano la umiliki wa milele.

Mika 4:6-8; Amosi 9:11,15; Ezekieli 37:21-22; Yeremia 23:3,8; Mwanzo 13:14-17; Waebrania 11:8-9; Wagalatia 3:16; Walawi 26:42; Mika 7:20; Isaya 11:12; Yeremia 31:10; Zekaria 8:8; Ezekieli 36:34-36.

27) Kuwa kuongezwa kwa agano lake na Ibrahimu, Mungu alifanya agano na Daudi, kwa utaratibu na hakika ya vitu vyote, akiahidi kuwa mzao wake, mzao maarufu (Pia akiwa mwana wa Baba wa milele) sharti aketi katika kiti cha (Page 13) Enzi cha Daudi, Kuwa auwawe na ainuke tena; kuwa Ufalme wake usiwe na mwisho; kuwa atatawala juu ya nyumba ya Yakobo milele, mbele ya uwepo wa Daudi mwenyewe. Kuwa haya maagano kuhusu nchi na Ufalme, yameandikwa na Paulo kama maagano ya ahadi, ambayo yakisha thibitishwa kwa damu ya Kristo katika kifo na ufufuo yanajumuisha Agano Jipya. Haya yanabeba vitu kuhusu Ufalme kama ilivyoelezwa na Kristo na mitume, ambavyo lazima viaminiwe kama sehemu ya Imani inayothibitisha.

2 Samueli 7:5-16; 1 Nyakati 17:4-14; Saburi 89:4,27-29,35-37; 132:11-18; Isaya 9:6-7; Matendo 2:30; 2 Samueli 23:5-7; Saburi 16:10; Luka 1:32, 33; Waefeso 2:12; Warumi 15:8; Mariko 16:15-16; Yeremia 31:31; Matayo 26:28; Waebrania 9:15.

28) Kuwa Enzi ya Daudi itakuwa tena enzi ya Yahweh Katika Mikono ya mfalme Yesu, na Iwe katika Yerusalemu ambayo hadi miisho hii utajengwa tena na kuwa jiji kuu na kiti cha serikali kuu ya ulimwengu.

1 Wafalme 2:11; 1 Nyakati 29:23; Isaya 9:7; Yeremia 3:17; 33:17; Zekaria 2:12; 6:13; Luka 1:32; Saburi 102:16; Isaya 2:2-4; Mika 4:1-4.

29) Kuwa Mfumo wa utawala utakao simamishw a utakuwa ni wa wana wa Mungu, Wayahudi na Mataifa wa vizazi vyote vitakavyositawishwa kwa ufufuo na kubadilika na Kujumuisha, Kristo Kama kiongozi wa muungano, Mzao wa Ibrahimu ambaye kwake Mataifa yote yatabarikiwa.

Saburi 22:28; 149:5-8; Isaya 9:6-7; Danieli 7:27; 12:2; Luka 13:28; 1 Wakorintho 6:2; Ufunuo 2:26, 3:21, 11:18; Waefeso 1:22; Warumi 9:7-8; Wagalatia 3:29;1 Wathesalonike 4:15-17; Yohana 5:28-29; 6:39-40; Luka 14:14; Matayo 25:34,46; Ufunuo 5:9-10.

30) Kuwa katika Kuonekana kwa Kristo, Kabla Kusimamishwa kwa Ufalme kutakuwepo ufufuo wa walio haki na wasio haki, hasa wale wanaojua mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa na kuitwa wawe chini yake. Hawa, wawe wamebatizwa au hawajabatizwa, waaminifu au wasio waaminifu, watajumuika mbele ya kiti chake cha hukumu pamoja na watakao kuwa hai wakisha kulisikia neno. Kila mmoja atatoa hesabu ya matendo yake mwenyewe, ili ahukumiwe kulingana na kazi yake na apate dhawabu ya vitu alivyovifanya katika mwili, Ikiwa ni mema au maovu.

2 Wakorintho 5:10; 2 Timoth 4:1; Warumi 2:5-6,16; 14:10-12; 1 Wakorintho 4:5; Ufunuo 11:18.

31) Kuwa waliohaki, baada ya hukumu, watabadilishwa miili inayokufa, ipatikanayo na uharibifu iwe isiyoharibika, kupitia kwa nguvu za Kristo, kwa "kufumba na kufumbua", Watatunukiwa heshima na kuinuliwa ili watawale pamoja na Yesu kama washirika katika kuurithi Ufalme, wamiliki wa dunia na watawala wa sheria ya Mungu miongoni mwa watu katika kila jambo. Wasio haki watakataliwa kwenye kiti cha hukumu kama "Waliolaaniwa", na baada ya "Kuteswa kwa Mapigo mengi au Machache", Kama vile. Mfalme atakavyowahukumu, wataharibiwa katika "Mauti ya pili", ambapo hakutakuwa na kuachiliwa tena.

1 Wakorintho 15: 51-55; 2 Wakorintho 5:1-4; Yakobo 1:12; Warumi 2:7; Matayo 5:5; Ufunuo 5:9; Danieli 7:27; 1 Wathesalonike 2:12; 2 Petro 1:11; Ufunuo 3:21; 2 Timotheo 2:12; Ufunuo 2:11; 5:10; Luka 22:29-30; Matayo 7:26,27; 8:12; 25:20-30; Danieli 12:2; Wagalatia 6:8; 5:21; 2 Wathesalonike 1:8; Waebrania 10: 26-31; 2 Petro 2:12; Malaki 4:1; Saburi 37:9,22,29-38; Mithali 10:25-29; Saburi 49:7-9; Ufunuo 20:14, 21:8.

32) Kuwa Ufalme wa Mungu utasimamishwa katika magofu ya utawala uliopo ambao utakataa kuwa chini ya Kristo. Utawala wa sasa utafanya mashauri ya pamoja ili kuenda kinyume na yeye, na mapinduzi yao yatatekelezwa na vita vya ile siku kuu ya Bwana wa Majeshi. Madhehebu yote ya upotovu yataondolewa na Bwana Yesu atakapochukua kisasi juu ya wale wasiomjua Mungu, pamoja

na kanisa la Warumi na dini zote zinazoyashika mafundisho yaliyo kinyume na neno la Mungu, pamoja na wale wanaoushika ukweli katika namna ya uovu na wanaoshiriki uasi kwa kujua. Haya yote ni “Majina ya Makufuru” yaliyoandikwa juu ya mnyama.

Danieli 2:44; Saburi 46:8-9; 2:1-12; Ufunuo 16:14; 2 Wathesalonike 1:7-10; Zekaria 13:3; Ufunuo 17 na 18; 19:2; 21:8; 17:3.

33) Kuwa sheria ya ulimwengu itatangazwa kutoka Yerusalemu Kama Amri takatifu kwa Mataifa, pasipo kufanya mashauri na watu, ili kuwaelekeza katika utakatifu, ambao utapelekea kuondolewa kwa vita na ulimwengu kujazwa na hali ya kuujua utukufu wa Yahwe kama maji yafunikavyo bahari. Kutokana na utaratibu huu mpya, wa vitu, familia zote za dunia zitabaikiwa kiroho, kiuongozi na kijamii, vile vile kimwili, kutokana na “utukufu kwa Mungu aliye juu”, ambayo itakuwa sheria ya kwanza ya Ufalme. Kutokana na haya, amani ya ulimwengu na utakatifu vitadumu kupitia kwa utawala wenye nguvu wa Kristo pamoja na watakatifu wake.

Isaya 2:3; Mika 4:2; Isaya 26:9; Saburi 46:9; 72:7; Isaya 2:4; Zekaria 9:10; Hesabu 14:21; Isaya 11:9; Habakuki 2:14.

34) Kuwa Ufalme wa Mungu utakao simamishwa katika mkono wa Kristo na watakatifu wake utaendelea kwa miaka elfu, ambapo dhambi itazuiliwa na kipindi cha Maisha kurefushwa miongoni mwa wakaazi wa dunia.

Ufunuo 20:4-9; 11:15; Isaya 65:20; Ezekieli 44:23,24; 1 Wakorintho 15:24-28.

35) Kuwa lengo la Ufalme litakuwa kuwapiga maadui wote na mwisho mauti yenyewe, kupitia kufungua njia ya uzima kwa Mataifa ambao wataingia kwa Imani wakati wa miaka elfu moja na kwa uhalisi katika kukamilika kwa miaka elfu. Matokeo yake yatakuwa mavuno makuu ya ukombozi mwishoni mwa miaka elfu, ambapo uharibifu utaondolewa kabisa miongoni mwa wanadamu.

Mwanzo 22:17,18; Saburi 47:3; 110:2; 1 Wakorintho 15:25-28; Saburi 67:2; Warumi 16:26; Ufunuo 14:6, Ufunuo 20 na 21.

36) Kuwa katika mwisho wa miaka elfu wa kutawala kwake Kristo, katiba ya Ufalme itabadilishwa kutokana na ufufuo na hukumu ya mwisho, ambapo wale watakaopatikana kuwa wenye haki watapewa uzima wa milele na watenda dhambi wataharibiwa na

kuondolewa katika Ufalme. Kutokana na haya, dhambi na mauti vitaondolewa duniani. Kisha Yesu Kristo ataukabidhi Ufalme wa Baba, ili Mungu awe yote katika wote, wanadamu wakiisha kurejeshwa katika urafiki na Muumba wao na Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao.

Ufunuo 20:11-15; 21:1-4; 1 Wakorintho 15:28; Saburi 132:13,14.

## KUHUSU JINA LAKE ESU KRISTO

Kuwa jina Yesu (Waebrania Y'shua) ambalo Mungu alifanya lijulikane kwa maria na yusufu, linamaanisha "Wokovu wa Mungu" kwa sababu mtoto ambaye angezaliwa "angewaokoa watu wake kutoka kwenye dhambi". Kristo sio jina bali ni cheo, kumaanisha mpakwa mafuta, katika kiebrania, Masihi, na hili linaonyesha kuwa Yesu angekuwa nabii, kuhani na mfalme.

Matayo 1:20; Luka 1:31; Luka 4;18; Matendo 10:38; Waebrania 1:9.

37) Kuwa Mitume waliagizwa na Yesu Kristo kuutangaza wokovu, ambao ni kiingilio katika Ufalme wa Mungu, katika jina lake, Jina Pekee lililopeanwa chini ya mbingu ambalo wanadamu sharti waokolewe; na kuwa hili tangazo lilifanyika kwanza kwa Wayahudi na kisha kwa Mataifa kutwaa miongoni mwao watu kwa jina lake.

Matayo 28:18-20; Mariko 16:15; Luka 24:46-48; Yohana 20:21; Matendo 10:42; 4:12; 3:26; 13:46; 15:14; Waefeso 3:5,6.

38) Kuwa kifungu ***"Jina lake Yesu Kristo"*** linaashiria Zaidi ya nafsi yake mwenyewe. Linalingana na ***"Jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu",*** na linaonyesha *"Siri kuu ya wema"* au lengo fiche la Mungu, ambalo ni Mungu kudhihirika katika mwili. Mungu alijifunua mwenyewe kupitia kwa umoja wa kibinafsi, mwanawe ambaye amechagua awe mkuu juu ya uumbaji mpya; na kisha amedhihirika (kwa kweli iliyoeleweka, ikaaminika na kuitii) katika wingi wa umoja kwenye mwili na damu asili, wale watembeao kwenye upya wa uzima. Umoja wa utakatifu binafsi, au neno kufanyika mwili, lilithibitishwa na roho pale Yesu alipotukuzwa; na wingi wa umoja, ukijumuisha wale walioteuliwa miongoni mwa wengi walioitwa, watakuwa kama yeye atakapoonekana kwenye utukufu. Hili litakapokami lishwa, "Jina" litakuwa Baba wa Milele atakayedhihirishwa kupitia kwa roho akiwa miongoni mwa jamii kuu

ya watauwa waume kwa wake ambao hakuna mtu awezaye kuhesabu.

Matendo 2:38; 8:12,16; Matayo 28:19; Acts 10:47,48; 19:5; 1 Timotheo 3:16; Yohana 1:14;17:6; 1 Wakorintho 6:20; 2 Wakorintho 5:19; 1 Yohana 1:1-2; 2 Wakorintho 4:6-7; 10-11; Waefeso 2:7,10; Warumi 8:17-19; 1 Yohana 3:1-2; 4:16; Ufunuo 7:9; 14:1.

39) Kuwa jina linakaa katika hali mbili, ya sasa na Ijayo. Katika hali ya sasa kidhabihu linalinganishwa na Mji Mtakatifu na madhabahu yaliyoganyagwa. Mungu ameweka jina lake katika mashiuika yake ambayo kupitia kwayo baraka zote zinatiririka na wale wanaoingizwa kwa jina wanakuua wafuasi wa mwili mmoja wa Kristo, ambao ni Eklesia. Katika hali Ijayo, Jina litaonyeshwa katika mfumo wa utawala kwenye Ufalme, likijumuisha ndugu na dada watukufu wa Bwana Yesu, watakaosimama kama bibi harusi aliyeposwa, mke wa Mwana Kondoo, Yerusalemu mpya.

Matendo 2:38; 8:16; 10:48; 19:5; 1 Wakorintho 12:13; Warumi 12:1-5; 1 Wakorintho 10:16-18;12:27; Waebrania 13:10; Ufunuo 6:9; 11:1;16:7; Waefeso 5:23; 2 Wakorintho 11:2; Wakolosai 1:18-19; Ufunuo 21:2, 9-10.

40) Njia ya kushiriki katika jina na kupata ushirika wa Baba na mwana ni, kuiamini injili iliyohubiriwa na Yesu na mitume, na kubatizwa, kwa njia ya kuzikwa katika maji.

Matayo 28:18-20; Matendo 8:37-39; Mariko 1:9-10; Warumi 6:4; Wakolosai 2:12.

41) Kuwa ubatizo ni ilani ya wazi ya kuamini ufufuo wa Mungu kwa mwana wake Yesu Kristo kutoka mauti, ni mfano wa kushiriki katika mauti, kuzikwa na kufufuka kwake Yesu ambapo hukumu ya kweli ya dhambi inatambuliwa, na dhambi za waumini zinatubwa na kusamehewa kwa Imani katika damu iliyomwagika ya Kristo. Katika njia hii, wanainuliwa tena kwa uadilifu na utakatifu ambao in upya wa uzima. Kwa hivyo ubatizo ni muhimu kwa ajili ya wokovu ulio jibu la dhamiri bora mbele ya Mungu.

Warumi 10:9-10; 3:24-25, 6:4-8; Matendo 2:38; 3:19; 22:16; Waefeso 2:13; Mariko 16:16; 1 Petro 3:21; 1 Yohana 1:7; Ufunuo 1:5.

42) Kuwa hakuna muumini wa injili aliyebatizwa na dhambi zake kusafishwa na kuondolewa, anaweza kuupokea utukufu na heshima na uhai usio na kikomo katika Ufalme wa Mungu,

asipokataa kibinafsi namna zote zisizo za kiMungu na tamaa za kidunia na kuishi katika kujizuia, kuwa kwenye utakatifu na kiMungu katika nyakati za sasa zenye uovu, akitazamia lile tumaini lenye baraka na, kuonekana kwake Mungu mkuu na mwokozi wetu Yesu Kristo, aliyejitoa kwa ajili yetu ili atuokoe kutoka namna zote zisizo za sheria na kujisafishia watu walionunuliwa kwa dhamana wenye shauku ya kazi bora.

Luka 9:23-26; Warumi 2:6,10; Tito 2:12,13; Yakobo 2:18-20; 2 Petro 1:5-10.

43) Kuwa hakuna wanaotambuliwa kama marafiki wa Kristo au ndugu isipokuwa wale waaminio yale aliyofundisha na KUFANYA yale ambayo ameamuru. Kwa hivyo, "Kuzikwa Kwenye Maji" Kunakotekelezwa na Madhehebu mengine ya KiKristo au miungano ambayo imetoka kwenye Imani moja hakusimami sio ubatizo mmoja na roho moja katika mwili mmoja wa Kristo. Watu wale ambao wamezikwa kwenye maji na labda wanapungukiwa katika kuilewa kweli kama ilivyo katika Yesu, au wale wanaojipata wamedanganywa kuyakubali mafundisho au mienendo iliyo kinyume na sheria ya Kristo, hawajashuhudia maungamo bora yanayohitajika na maandiko, na kwa hiyo hawawi sehemu yoyote ya mwili mmoja wa Kristo, kwani hakuna uongo ulio wa ukweli.

Yohana 15:14; 1 Yohana 2:18-19; 2 Timotheo 4:1-4; Yuda 17-19; 2 Yohana 1:9-11; 2 Petro 2:14-22; 1 Yohana 2:21.

44) Kuwa Kuzikwa tena kwa maji kwa wale watu ambao baadaye wanafanya maungamo bora si kubatizwa tena, bali ni kabatizwa kwa kwanza katika mwili mmoja wa Kristo yanavyohitaji maandiko.

Matendo 19:1-5; Waefeso 4:5.

45) Kuwa mwili wa Kristo ni neno linaloeleza juu ya Eklesia, ambalo linasimamia waumini wote waliobatizwa kila mahali na kila taifa pasipo kuzingatia rangi, ambao wameonganishwa juu ya msingi wa kuikubali Imani moja, wanaomwogopa Mungu na kumpenda na kujitahidi kufanya yaliyo kweli na yanayokubalika kwa macho yake. Eklesia pia inaelezwa kwa neno la Mungu kama muungano wa waumini waliobatizwa katika sehemu yoyote ile ambao wanawakilisha mwili mmoja wa Kristo kwa ulimwengu na wanatambuliwa kuwa ni nyumba ya Mungu, nguzo na msingi wa ukweli. Waumini wote wa Eklesia ya Pahali Maalum wanawajibika

kwa Kristo kama kichwa cha mwili, na wanawajibikiana wao kwa wao kwa maslahi ya Eklesia ile Pasipo kuwapendelea watu Fulani.

Waefeso 5:23,27; Wakolosai 1:18; 3:15; Warumi 12:5; 1 Wakorintho 12:13,27; Waefeso 2:18-22; Yuda 3; 1 Wakorintho 1:2; 1 Wathesalonike 1:1; 1 Timotheo 3:15; 1 Wakorintho 12:25-27, Yakobo 2:1.

46) Kuwa kutaniko la kila juma kwa tendo la kumkumbuka Bwana Yesu linahitajika kwa marafiki wote wa Kristo. Kwa usawa na sheria ya Kristo na mienendo ya mitume, wanafaa **"Kutangaza mauti yake hadi kuja kwake"** kwa kuumega mkate na kuinywa divai pamoja. Kushiriki katika hiki kitendo cha ukumbusho ni kushiriki katika meza ya Bwana na wote ambao wanafanya hivi ni sawa mmoja kwa mwingine katika kitendo kikuu cha ushirika. Huu mwenendo unafaa uzingatiwe barabara na wafuasi wote wa mwili wake.

Matendo 20:7; 1 Wakorintho 16:2; Luka 22:19,20; 1 Wakorintho 11:23-28; 1 Wakorintho 10:21; 1 Wakorintho 10:16,17; 2 Wathesalonike 2:15.

47) Kuwa wafuasi wa Eklesia, Kama wenyeji wa Ufalme wa Mungu, wanamtambua bwana mmoja tu na wanawiwa utiifu wao kwa Yesu Kristo Pekee. Kwa hivyo hawawezi toa kiapo cha utiifu kwa mamlaka tawala yoyote ya ulimwengu. Hawaruhusiwi "Kutwaa upanga" kwa kutumikia majeshi ya taifa lolote kwa sababu Kristo amekanya hilo. Wakati wanawekwa chini ya amri ya binadamu, kwa ajili ya Kristo, (Isipokuwa mahali amri inaenda kinyume na sheria ya Kristo) hawaruhusiwi kutoa sheria, kama mahakimu au Askari, au kutumika kama wanasheria, wakiamriwa kuuwa, bila kukaidi uovu, au kuhukumu. Wanapoamriwa kujitenga na ulimwengu, hawafai kushiriki katika siasa, au kuwa kwenye vyama vya wafanyikazi, wakitambua kuwa hakuna mtu awezaye kuwatumikia mabwana wawili.

Wafilipi 3:18; Matayo 23:8-10; Matayo 6:24; Luka 16:13; Matayo 5:34; Yakobo 5:12; Matayo 26:52; Warumi 13:9; Matayo 5:39; Luka 6:37,38; 12:13,14; Yohana 7:24; 1 Wakorintho 5:11-13, 2 Wakorintho 6:14-18.

# MAFUNDISHO YANAYOFAA KUKATALIWA

"Kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka Mbinguni juu ya uasi wote na uovu wa wanadamu waipingao kweli kwa uovu…."

Warumi 1:18

1) Kuwa Bibilia ni kazi ya pumzi ya Mungu kwa sehemu tu au Ikiwa ni yote, basi ina Makosa ambayo pumzi ya Mungu imeruhusu kuwepo.

*Maandiko yanayopinga:* 2 Timotheo 3:16; 2 Petro 1:21

2) Kuwa Mungu ni nafsi tatu.

*Maandiko yanayopinga:* Kumbukumbu 6:4; Isaya 45:5,6,18; 46:9; Marko 12:29; 1 Wakorintho 8:6; Waefeso 4:6; Yohana 17:3; 1 Timotheo 2:5.

3) Kuwa Yesu alikuwa Mungu Mwana, aliye wa kiwango sawa na utukufu sawa na Baba.

*Maandiko yanayopinga:* Luka 1:35; Matendo 2:22; Yohana 15:10; Matayo 3:17; Yohana 5:30; 14:28; 8:42; 7:16; 1 Yohana 4:9; 1 Wakorintho 11:3; 1 Wakorintho 15:28.

4) Kuwa Roho Mtakatifu ni mtu kibinafsi kando na Baba.

*Maandiko yanayopinga:* Luka 1:35; Isaya 11:2; Yohana 3:34; 20:22; Matendo 10:38; 8:11-20; Isaya 44:6,8; 45:5,21; Hosea 13:4; 1 Wakorintho 11:3.

5) Kuwa Mungu alitumia njia zisizo na utaratibu za mageuzi kuziumba mbingu na nchi, vilevile na viumbe wote kwa kipindi cha muda mrefu.

*Maandiko yanayopinga:* Mwanzo 1:1; Mwanzo 1:24-31; Kutoka 20:11; Isaya 40:12-13; Ayubu 38:4,6; Yeremia 31:35; Matayo 19:4-5; Mariko 10:6.

6) Kuwa Kristo alizaliwa na "Uhai huru".

*Maandiko yanayopinga*: Warumi 5:18,19; 1 Wakorintho 15:21; Warumi 1:3; Waebrania 2:16; Isaya 53:3,4.

7) Kuwa Asili ya Kristo ilikuwa Isiyo na mawaa, kwa hivyo hakowa na mwili sawa kama wa ndugu zake.

Maandiko yanayopinga: Isaya 53:4, 2 Wakorintho 5:21; Wagalatia 4:4; Warumi 1:3; Waebrania 2:10,14-15; 4:15; 5:7-8.

8) Kuwa Yusufu alikuwa baba halisi wa Yesu.

*Maandiko yanayopinga*: Matayo 1:18,20,24,25; Luka 1:34,35; 3:23; Mwanzo 3:15; 2 Samueli 7:14; Isaya 7:14.

9) Kuwa Mwanadamu hahukumiwi kwa hesabu ya asili yake ambayo ni dhambi ya mwili.

*Maandiko yanayopinga:* Warumi 7:18,25; 8:3; Waefeso 2:3; Warumi 6:6,9.

10) Kuwa mtu anayo roho isiyokufa.

*Maandiko yanayopinga:* Isaya 10:18; 53:10; Ezek 18:4; Saburi 22:29; 78:50; 89:48; 49:8.

11) Kuwa mtu huendelea kuishi katika mauti.

*Maandiko yanayopinga:* Ayubu 3:13,19: Saburi 115:17; Saburi 146:3,4; Mhubiri 9:5-10; Saburi 6:5; Isaya 38:18,19.

12) Kuwa waovu watateswa mateso ya milele katika Jehanamu.

*Maandiko yanayopinga:* Ayubu 3:17; Mhubiri 3:20; 2 Wathesalonike 1:9, Saburi 37:20; Saburi 49: 6-20.

13) Kuwa watakatifu huenda Mbinguni baada ya kufa, au hupaa kuingia katika Ufalme ulio Mbali na mbingu wanapokufa, au huenda kuwa na Yesu.

*Maandiko yanayopinga*: Matayo 6:10; Matayo 5:5; Danieli 7:27; Matendo 2:29, 34; Yohana 3:13; Warumi 4:13; 1 Petro 1:13; Waebrania 11:39,40; Ufunuo 5:9,10.

14) Kuwa “Wakristo wa kweli”, Watakaokuwa wakiishi wakati wa kuja kwake Yesu watanyakuliwa hadi mbinguni katika “Uhamisho” wa mitume na dunia ya sasa itachomwa na kuharibiwa.

*Maandiko yanayopinga:* Dan 7:18,27; Ufunuo 11:15; Yohana 5:28-29; 2 Wakorintho 5:10; Saburi 78:69; 104:5; Mhubiri 1:4; Isaya 45:18; Matayo 5:5; Matayo 6:10.

15) Kuwa “Mpinga Kristo”, hataonekana mpaka miaka saba ya mwisho ya utawala wa binadamu.

*Maandiko yanayopinga:* 1 Yohana 2:18,22; 4:3; 2 Yohana 7.

16) Kuwa “Ibilisi” au “Shetani” ni kiumbe binafsi Zaidi ya mwanadamu kiletacho majaribu.

*Maandiko yanayopinga:* Waebrania 2:14; Yakobo 1:13-14; 4:7; Mariko 7:20-23.

17) Kuwa Ufalme wa Mungu ni “Kanisa” na kuwa Kristo aliteua daraja la kipekee la “Makuhani” au maaskofu kutawala na kuwaombea dua waumini wa kawaida.

*Maandiko yanayopinga:* Dan 2:44; Mika 4:1-8; Matayo 6:10; 19:24; 21:43; Luka 13:28-29; 21:31; Matayo 23: 8-10; 1 Timotheo 2:5; 1 Petro 1:1,2; 2:5,9.

18) Kuwa injili inahusu kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu pekee.

*Maandiko yanayopinga:* Mariko 1:14; Luka 18:31-34; Matendo 8:12; 28:31; Wagalatia 3:8; Waebrania 4:2.

19) Kuwa Kristo hatarudi mpaka itimie miaka elfu.

*Maandiko yanayopinga:* Ufunuo 16:15, Ufunuo 20:4.

20) Kuwa unabii wa kitabu cha ufunuo utatimizwa baada ya kurudi kwake Yesu Kristo, au ulitimia wote zamani.

*Maandiko yanayopinga:* Ufunuo 1:1; 1:19; 11:15-19; 13:7,8; 16:15; 17:9-11.

21) Kuwa baraka za kipekee zilizoahidiwa kwa mujibu wa kukielewa kitabu cha ufunuo wa Yesu Kristo, hakina mtajo wowote kuthibitisha uzima.

*Maandiko yanayopinga*: Ufunuo 1:3; 2:7,10,11,17,25,26; 3:5,12,21; 13:8-10; 16:1; 22:6-7.

22) Kuwa Kristo hatawahukumu watakatifu wakati wa kuja kwake, bali atagawa miongoni mwao viwango tofauti vya tuzo na kuwa hawatahitajika kutoa hesabu ya matendo ya kuishi kwao wakati atakaporudi.

*Maandiko yanayopinga:* Matayo 12:36-37; 18:23; Warumi 14:12; 1 Petro 4:17-18; 2 Wakorintho 5:10.

23) Kuwa ufufuo ni wa waaminifu pekee.

*Maandiko yanayopinga:* Danieli 12:2; Yohana 5:29; Matendo 24:15; 2 Wakorintho 5:10.

24) Kuwa wafu watafufuka katika hali ya kutokuharibika.

*Maandiko yanayopinga:* Yohana 5:21; 28-29; 20:17; Warumi 14:9; 1 Wakorintho 15:53; 2 Wakorintho 5:10; Wafilipi 3:21.

25) Kuwa Mataifa yatakayokuwa chini ya Ufalme wakati wa miaka elfu yatakuwa yasiyopatwa na uharibifu.

*Maandiko yanayopinga:* Isaya 65:20; Ezekieli 44:25; Ufunuo 20:5,8-10,12-13, 15; 1 Wakorintho 15:26.

26) Kuwa sheria ya musa inafungamanisha waiaminio injili.

*Maandiko yanayopinga*: Warumi 3:9; 7:6; Wagalatia 5:4.

27) Kuwa kuishika siku ya saba au siku ya kwanza ya Juma (Jumapili) Kama. Sabato ni lazima ili kupata wokovu.

*Maandiko yanayopinga*: Warumi 14:5-6; Wagalatia 4:10,11; Wakolosai 2:16.

28) Kuwa kuna nyama zifaazo kukataliwa kwa kigezo cha kuwa najisi.

*Maandiko yanayopinga*: Warumi 14:14-17; Wakolosai 2:16; 1 Timotheo 4:3.

29) Kuwa Ahadi kwa Ibrahimu na Daudi zilitimizwa wakati nchi ya Kanani ilikaliwa na Wayahudi chini ya sheria ya musa.

*Maandiko yanayopinga*: Matendo 7:5; Waebrania 11:13.

30) Kuwa “Wokovu” ni hali inayotimizwa mara moja kutokana na kazi ya Roho Mtakatifu moyoni.

*Maandiko yanayopinga*: Matayo 10:13,24:13; Mariko 16:16; Matendo 11:14; Warumi 5:9-10; 1 Wakorintho 15:2; 1 Timotheo 4:16; 1 Petro 3:21.

31) Kuwa wanadamu wameazimiwa wokovu pasipo masharti.

*Maandiko yanayopinga*: Luka 13:24; Warumi 2:7; Wafilipi 2:12; 1 Wakorintho 9:27; 2 Timotheo 2:5,10; Waebrania 3:12-14.

32) Kuwa ni sharti mtu kupokea Roho Mtakatifu ili aweze kuelewa maandiko.

*Maandiko yanayopinga*: Matendo 8:12-15; Warumi 10:17.

33) Kuwa Mwanadamu anaweza kuokolewa kupitia kwa uadilifu na unyofu pasipo kuijua Injili au Habari, Njema jingi ilivyo katika Maandiko.

*Maandiko yanayopinga*: Mariko 16:15,16; Yohana 6:40; Matendo 4:12; Warumi 1:16; 2 Wathesalonike 2:13; Waebrania 11:6.

34) Kuwa Imani pekee yatosha kwa wokovu.

*Maandiko yanayopinga*: Yakobo 2:14,17,20,24; 2 Petro 1:5-11.

35) Kuwa wasiojua, wasioelimishwa na wale wasioweza kuelewa, pamoja na Watoto wadogo, watashiriki katika jumuia ya ufufuo na kuokoka, pasipo na hekima ya kuiamini injili kama sharti.

*Maandiko yanayopinga*: Yohana 20:31; Waebrania 11:6.

36) Kuwa kuijua injili kutaokoa pasipo kuzitii sheria za Kristo.

*Maandiko yanayopinga*: Yakobo 2:20,26; Luka 13:26,27; 1 Petro 4:17; 2 Wathesalonike 1:8.

37) Kuwa ubatizo si lazima ili kupata wokovu.

*Maandiko yanayopinga*: Mariko 16:15,16; Yohana 3:5; Matendo 2:38; 10:47,48; 22:16; Wagalatia 3:27; Wakolosai 2:12; 1 Petro 3:21; Yohana 15:4.

38) Kuwa kurashia Watoto maji ni ubatizo kwa mujibu wa Maandiko.

*Maandiko yanayopinga*: Matendo 8:38,39; Waromi 6:4; Wakolosai 2:12.

39) Kuwa kuelewa injili kikamilifu si lazima kuufanya ubatizo kuwa dhabiti.

*Maandiko yanayopinga*: 2 Wakorintho 4:3-4; Mariko 16:16.

40) Kuwa kuzikwa kwenye maji kunakofanywa na madhehebu (kafiri) kunaweza kuunganisha kwa mwili wa Kristo.

*Maandiko yanayopinga*: 2 Timotheo 3:8; Tito 1:16; 2 Petro 2:1; Ufunuo 2:23.

41) Kuwa "Mwili mmoja wa Kristo" unahusu tu wakati ujao na hali kamilifu.

*Maandiko yanayopinga*:1 Wakorintho 10:17; Warumi 12:5; Waefeso 4:4; Wakolosai 3:15.

42) Kuwa uzao wa "Anglo-Saxon" ni kabila kumi za Israeli ambazo kufaulu kwake ni kutimizwa kwa ahadi alizopewa Efraimu.

*Maandiko yanayopinga*: Amos 3:2; 2 Wafalme 17:6; Mwanzo 35:12; Warumi 4:16,17.

43) Kuwa Ndugu wa Kristo hana wajibu wowote kwa Eklesia yake mwenyewe.

*Maandiko yanayopinga*: Yohana 13:14; Warumi 15:1; 1 Wakorintho 10:24; 12:25-26; 2 Wathesalonike 1:3; 1 Petro 1:22; 5:2; 1 Yohana 3:16; Waebrania 10:25.

44) Kuwa wanawake wanaweza kufundisha na haistahili wawe kimya katika Eklesia, haistahili wafunike vichwa vyao katika Ibada, na kuwa hakuna aibu yoyote kunyolewa nywele zao.

*Maandiko yanayopinga*: 1 Wakorintho 14:34; 1 Timotheo 2:11-12; 1 Wakorintho 11:3-10.

45) Kuwa Ndoa na wasioamini Inaruhusiwa kisheria.

*Maandiko yanayopinga*: 2 Wakorintho 6:14; 1 Wakorintho 7:39.

46) Kuwa talaka na kuoana tena vinaruhisiwa chini ya sheria ya Kristo.

*Maandiko yanayopinga*: Matayo 19:9; Luka 16:18; 1 Wakorintho 7:10-11.

47) Kuwa kutengwa ghafla na mtu au Eklesia pasipo kuonya au kukaripia kihalali kunahesabiwa haki chini ya sheria ya Kristo.

*Maandiko yanayopinga*: Matayo 18:15-17; Matendo 15; Tito 3.10.

48) Kuwa haiwezekani kutambua ukweli kutoka kwa Maandiko Matakatifu pekee pasipo kuzingatia Ushahidi Mwingine wa kawaida.

*Maandiko yanayopinga*: Yohana 8:32; 17:17; 2 Petro 1:2-3; Mithali 30:6; Matayo 15:9; Yohana 14:26; 2 Timotheo 3:15-17.

49) Kuwa waumini wana uhuru wa *a)* Kutumika katika Jeshi na huduma ya ulinzi wa taifa katika ngazi yoyote; *b)* Kutumika kama maafisa wa polisi *c)* au kutoa kiapo cha uaminifu kwa Mtawala yeyote wa ulimwengu *d)* kutumika kama wanasheria au *e)* Kushiriki katika uongozi wa wafanyakazi au siasa.

*Maandiko yanayopinga*: Saburi 1:1; 26:4-5; Yeremia 17:5; Matayo 5:34-39; 26:52; 2 Wakorintho 6:14-17; Waefeso 2:19; 4:17; 5:7-11; Warumi 12:2,19; 2 Wakorintho 6:17; Wafilipi 1:27; 3:20; 1 Wathesalonike 5:15; 2 Timotheo 2:22; Yakobo 5:12.

50) Kuwa waumini wana uhuru kuchukua hatua kisheria kwa sababu yoyote au kilipwa deni kupitia njia ya kulazimu kisheria.

*Maandiko yanayopinga*:1 Wakorintho 6:1-7; Matayo 5:39-40; Luka 6:29-30; Warumi 12:19.

51) Kuwa mafundisho ya Maandiko kuhusu ushirika, si nguzo muhimu au ukweli na kuwa si Lazima kujitenga na walimu potofu au ndugu wasio waaminifu wakataao maonyo.

*Maandiko yanayopinga*: Matendo 2:42; 1 Yohana 1:1-7; 2 Wathesalonike 3:14,15; Warumi 16:17; 2 Wathesalonike 3:6; 1 Wakorintho 5:5-7; 2 Yohana mistari 8-10; 1 Timotheo 6:3-5; Tito 3:10; 2 Wathesalonike 3:10; 1 Tim 5:8.

52) Kuwa wateule wanaweza kupatikana miongoni mwa madhehebu yote au kadhaa pasipo kudumisha hali ya kujitenga katika wakati wa sasa, kushindana wenyewe, na kutokuelewana kimafundisho miongoni mwao wenyewe.

*Maandiko yanayopinga*: 1 Wakorintho 1:10; 3:3; 12:25; Waefeso 4:3-6; Wagalatia 1:6-9.

**"--- na likiwepo neno lolote lisilopatana na mafundisho yenye uzima"**

1 Timotheo 1:10

# S H E R I A  Z A  K R I S T O

## Z I K I T E K E L E Z W A

**WAKAO NDANI YA IMANI ULIMWENGUNI**

**KOTE HATA**

**NA VIZAZI VYA BAADAYE**

"Nyinyi ni marafiki zangu ikiwa mwatenda yote ninayowaamuru." – Yesu

"Wafundishe kuyashika mambo yote ambayo nimewaamuru." – Yesu

"Ikiwa mwayajua haya mambo, heri ninyi, ikiwa Mwayatenda." – Yesu

"Si Kila aniitaye, bwana, bwana, ataingia katika Ufalme, bali yule atendaye mapenzi ya Baba yangu." – Yesu

"Muwe watendaji wa neno, wala si wasikiao tu, mkijikana nyinyi wenyewe." – Yakobo

"Yule asemaye, Namjua, wala hazishiki sheria zake,
ni muongo." - Yohana

# UTANGULIZI

*(kwa nakala ya kwanza)*

ELIMU YA DINI ya halaiki imepunguza sheria za Kristo na mitume wake kuwa zisizofaa kwa kazi yoyote. Imetia giza kabisa nguzo ya utiifu kama msingi wa kukubaliwa na Mungu katika Kristo, kwa. Mafundisho yake ya “kuthibitika kwa imani pekee” na pia kuwa, namna ya kutoweka upesi katika saa ya kifo. Elimu hii ni sehemu ya ukombozi wa kisasa wa njia za kale za mitume, kutambua dhahiri, kuwa ingawa imani humbadilisha mtenda dhambi kuwa mtakatifu, na utiifu pekee utahakikisha kukubaliwa kwa huyu mtakatifu mbele ya kiti cha hukumu; na kuwa mtakatifu asiyetii atakataliwa wazi zaidi ya mtenda dhambi asiyehesabiwa haki.

Sheria au kanuni ya utiifu inapatikana katika sheria za Kristo. Kristo anena wazi juu ya swala hili katika Maelezo yaliyonakiliwa. Kwenye ukurasa ujao. Yamewekwa pamoja katika huu usemi wake – “Ikiwa mtazishika sheria zangu, nyinyi mtadumu ndani ya upendo wangu”.

Kabla ya kuzishika sheria zake, ni sharti kuzijua; na ili tuzijue kwa lengo lolote, lazima tuweze kuzikumbuka. Huu muhtasari umenuiwa kuwa msaada wa ufahamu. Sheria zimechukuliwa kutoka kwa maandiko ya mitume, na kupangwa kwa njia mwafaka iwezeshayo kukumbuka, na kuchapishwa katika mfumo mwafaka wa kutekelezwa kwa mtu kila siku, ili ziweze kuangailiwa mara kwa mara, na kuchapishwa kwenye ubongo. Marejeleo yametolewa kuwatosheleza wale walio na ari ya kuwa na uhakika wanaume na wanawake wanaozishika amri hizi zote! Wako wapi? Bwana, ongeza idadi yao.

ROBERT ROBERTS

Birmingham, Juni 16, 1882

MUHTASARI WA

# SHERIA ZA KRISTO

Abamo zimejumuishwa sheria za mitume wake, kuhusu yale aliyoyasema “yeyote awasikiaye nyinyi, anisikia mimi”, na Paulo, “Mambo ninayowaandikia ni sheria za Bwana.”

## KUMHUSU MUNGU

**1) Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, roho, nguvu, na akili.** (Matayo 22:37)

**2) Mwogope Yule awezaye kuharibu roho na mwili katika “Jehanamu”.** [Mahali taka zilichomwa] (Matayo 10:28)

**3) Utukufu kwa Bwana; wala si kwa mwanadamu.** (1 Wakorintho 3:21; 2 Wakorintho 10:17)

**4) Muweze Kumuiga Mungu; Muwe kama yeye Katika wema wake kwa wasio haki.** (Matayo 5:45-48; Waefeso 5:1)

**5) Muombe Mungu siku zote nbila kufifia.** (Luka 18:1; Matayo 7:7; 26:41; Waefeso 6:18; Wafilipi 4:6; Wakolosai 4:2; 1 Wathesalonike 5:17; 1 Timotheo 2:8; Waebrania 4:16); **omba kwa unyofu na maneno machache** (Matayo 6:7); **omba kwa siri.** (Matayo 6:6)

**6) Kuwa na imani kwa Mungu; mtwike mizigo yenu; anajua genu na atawatimizia.** (Mariko 11 :22; Matayo 6:25; Wafilipi 4:6; 1 Petro 5:7)

**7) Jitoeni miili yenu kumtumikia bila kukawia, mkitambua kuwa hamwezi kumtumikia Mungu na Mali** (Matayo 6:24; Warumi 12:1). **Jilindeni nafsi zenu na miunqu.** (1 Yohana 5:21)

**8) Kwa kila jambo, Toeni shukrani kwake, Maana haya ndio Mapenzi yake na ridhaa yake kwenu.** (Waefeso 5:20; Wakolosai 3:15, 17; 1 Wathesalonike 5:18; Waebrania 13:15)

**9) Mtambue yeye katika njia zako zote; ukinena kuhusu lengo lako “ikiwa yampendeza Bwana”.** (Yakobo 4:15; Mithali 3:6)

**10) Jitoe Katika ulimwengu na mjitende kwa ajili yake, kama wana na binti zake.** (2 Wakorintho 6 :14-1)

## KUMHUSU KRISTO

**11) Wacha Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani.** (Waefeso 3:17)

**12) Mpeni nafasi kuu zaidi ya Baba, Mama, mume, mke, watoto, jamaa, nyumba na mashamba.** (Luka 14:26; Matayo 10:37)

**13) Weka upendo wako kwake, na wala si kwa ulimwengu wa sasa kamwe.** (Wakolosai 3 :1-4; 1 Yohana 2:15)

**14) Mchukueni kama mfano na mfwate nyayo zake.** (1 Petro 2 :21-23; Yohana 13:15)

**15) Dumuni ndani yake: msimwache atoke katika mawazo yenu na mwenendo.** (Yohana 15:7; Waebrania 2:1)

**16) Mkumbukeni Kila siku ya kwanza ya juma katika kuumega mkate, kama anavyoagiza.** (Matayo 26:26-27; 1 Wakorintho 11:24-26; Matendo 2:42; 20:7; 1 Wakorintho 16 :2)

**17) Usione aibu kumkiri yeye mbele ya watu,** (Luka 12:8; Mariko 8:38; 2 Timotheo 1:8) **kwa wakati huo ukitahadhari kuonyesha mambo yako ya utakatifu kwa walio najisi.** (Matayo 7:6)

**18) Azimia kuwa tayari mara kwa mara kwa qjili ya kuja kuwake. Kwa kuzingatia hili, ukijiepusha na shughuli za kibiashara, wasiwasi wa maisha, na tamaa za anasa.** (Matayo 24:42-50; Luka 12:35-37; 14:26; 2 Petro 3:14)

**19) Vumilieni hadi mwisho, mkiridhia hali ngumu ikiwa yafaa.** (Matayo 24:13; 2 Timotheo 2:3)

**20) Shikilieni ujasiri wenu na kufurahi, katika Kristo Yesu hadi kifo au hadi kurudi kwake.** (Ufuno 2:10-25; Waebrania 3:14)

## KUHUSU NDUGU NA DADA

**21) Mpende jirani yako kama nafsi yako.** (Matayo 22:39; Mariko 12:31; Luka 10:27; Warumi 13:9; Wagalatia 5:14; Yakobo 2:8) **Mpendane nyinyi kwa nyinyi kwa moyo safi wenye bidii.** (Yohana 13:34; Warumi 12:10; Waefeso 5:2; Wakolosai 3:14; 1 Wathesalonike 4:9; Waebrania 13:1; 1 Petro 1:22; 1 Petro 4:8; 1 Yohana 3:14-19).

**22) Ndugu wasiwe wakuu juu ya ndugu wenzao; Aliye mkuu awe kama mdogo; msimamizi awe kama mtumishi; mfano wa Kristo waonyesha yanayokusudiwa.** (Matayo 23:11; Luka 22:26-27; Yohana 13:13-17)

**23) Msiwe wenye hasira pasipo sababu madhubuti; na msiishikilie hadi iwapelekee kutenda dhambi.** (Matayo 5:22; Waefeso 4:26; Wakolosai 3:8).

**24) Ikiwa kuna ugomvi, tafuta suluhu au Maridhiano na Kuwa na Msamaha ndilo lililo muhimu zaidi.** (Matayo 5:24; 18:35; Wakolosai 3:13)

**25) Ikiwa kuna dhambi (ijulikanayo au iliyosikiwa) usiitanqaze Kwa wengine bali umweleze ndugu aliyekosa kuhusu lile jambo baina yako na yeye pekee, kwa lengo la kusawazisha.** (Matayo 18:15; Wagalatia 6:1; Yakobo 5:19-20)

**26) Musinun'gunike wala kulalamika miongoni mwenu, au kuhukumu nia za mmoja wenu Msilaumiane nyinyi kwa nyinyi.** (Matayo 7:1-2; Warumi 14:13; 1 Wakorintho 4:5; Yakobo 4:11; 5:9) **Ikiwa yahitajika, hukumuni matendo maovu kudumisha upole na kuogopa.** (Warumi 2:3; 1 Wakorintho 5:9-13; Wagalatia 6:1).

**27) Usimzibie sikio lako mwenye uhitaji, wasaidieni wale wanaoumia na kusumbukana.** (Matendo 20:35; Warumi 12:13; Yakobo 2:16; Wagalatia 6:10; 1 Yohana 3:17)

**28) Usiwaze tu juu ya Maslahi yako mwenyewe, au kuubeba mzigo wako tu, bali ujali na mizigo ya wengine.** (Wafilipi 2:4; 1 Wakorintho 10:24; Wagalatia 6:2)

**29) Muwe na wazo moja, na mfuate mambo yaletayo amani.** (1 Wakorintho 1:10; 2 Wakorintho 13:11; 1 Petro 3:8; Warumi 14:19)

**30) Ungama makosa yenu mmoja kwa mwingine kwa jinsi; ya kutendana.** (Yakobo 5:16)

## KUHUSU MGENI

**31) Wacha nuru yenu iangaze mbele ya watu.** (Matayo 5:16; 10:32,33). **Singatia sana neno la uzima.** (Wafilipi 2:16). **Waambieni wanaopotea, Njoo.** (Ufumo 22:17).

**32) Patana na mshitaki wako upesi, mkikubali kutendewa uovu kwa ajili ya amani.** (Matayo 5:25; 1 Wakorintho 6:7; Warumi 12:18-19)

**33) Watendeeni mema watu wote kwa kadri ya hali inavyokuruhusu. Msamaria alimsaidia mgeni katika dhiki: "Enendeni mkafanye hivyo". Mfanye vivyo hivyo adui yenu ana njaa, mlisheni; akiwa na**

**kiu, mpeni kinywaji.** (Wagalatia 6:10; Luka 6:27-28; 10:37; Warumi 12:20; Matayo 5 :44)

34) **Waombeeni wanaowadhulumu na kuwachukia na hata kuwatesa.** (Matayo 5:44)

35) **Usilipize kwa mtu awaye yote uovu kwa uovu.** (Warumi 12:17; 1 Wathesalonike 5:15) **Usitwae kisasi, kurejesha vovu kwa vovu au kujibizana kwa lugha ya matusi, kinyome na haya, bariki, ukionyesha wema** (1 Petro 3:9); **bariki na wala vsilaani.** (Warumi 12:14)

36) **Usishindanie uovu; usilazimishe kurejeshewa kwa mali iliyoibwa; usichukue kisasi wewe mwenyewe, bali weka kwa hesabu ya Mungu.** (Matayo 5:39-40; Luka 6:29-30; Warumi 12:19)

37) **Usikubali uovu ukutawale, lakini shinda uovu kwa wema.** (Warumi 12:21)

38) **Jinsi unavyotaka watu wakutendee, nawe watendee vivyo.** (Matayo 7:12; Luka 6:31)

39) **Usitembee kama watembeavyo Mataifa** (Waefeso 4:17) **Usiwe na ushirika na kazi za giza zisizozaa matunda** (Waefeso 5:7-11): **Usipatanishwe na ulimwengu huu** (Warumi 12:2); **Jiondoe miongoni mwao na ujitenge.** (2 Wakorintho 6:17)

40) **Tembea kwa uaminifu kwa wale washiokuwa nacho, usitoe nafasi kwa adui kunena shutuma, usilaumiwe wala kudhulumiwa, muwe kama wana wa Mungu kati ya kizazi kaidi na kilichopotoka.** (1 Wathesalonike 4:12; 1 Timotheo 5:14; Wafilipi 2:15)

## KUHUSU MWENENDO WAKO MWENYEWE

41) **Uwe mtakatifu katika namna yote ya maongezi** (1 Petro 1:15-16); **pasipo utakatifu hakuna mtu atakayemuona Bwana.** (Waebrania 12:14)

42) **Iweni werevu kama nyoka, na wapole kama njiwa** (Matayo 10:16; Wafilipi 2:15): **si wapumbavu** (Waefeso 5:15-17): **wapole, watiifi, wenye moyo mwema, wenye huruma, wenye rehema, wenye kusamehe.** (2 Timotheo 2:24; Tito 2:2; Waefeso 4:32; Wakolosai 3:12; Matayo 18:35).

43) **Wazee kwa watoto wawe wenye ukweli, wenye busara, wanyofu na wenye kujizuia.** (Wafilipi 4:5; Tito 2:2,7; 1 Petro 1:13; 5:8)

44) **Kuwa wenye bidii katika kuyatenda mambo yote yanayompendeza Mungu "Lolote mfanyalo, fanyeni kwa bidii kama kumfanyia Bwana na wala si wanadamu".** (Warumi 12:1-2; Wakolosai 3:23)

45) **Kuwa wenye kulinda; kukesha, wajasiri, wachangamfu, wenye adabu na wenye kuheshimika.** (1 Wakorintho 16:13; Wafilipi 4:4; 1 Wathesalonike 5:6, 8,10; 2 Petro 1:5-7)

46) **Iweni wenye huruma kwa wengine katika dhiki na furaha yao.** (Warumi 12:15)

47) **Nyinyi nyote muweze kuvikwa unyenyekevu, wala sio dharau, pasipo kujali vitu vya hali ya juu, bali kuwatendea wema watu wa nafasi; za chini.** (Luka 14:11-13; Warumi 11:20; 12:3-16; Wafilipi 2:3; Wakolosai 3:12; 1 Petro 5:5-6)

48) **Iweni wastahimilivu kwa kila mmoja, hasa wanyonge, wasio na uhakika na wenye kusitasita** (Warumi 12:10; 14:1, 15:1; 1 Wathesalonike 5:14); **Wekeni mbali hasira, ghadhabu, ukali na maongezi ya uovu yote.** (Wafeso 4:31; 1 Petro 2:1)

49) **Fuateni mambo yote yaliyo kweli, aminifu, haki, safi, kupendeza, adilifu, mema, na sifa njema.** (Wafilipi 4:8); **Chukieni uovu na muachane na hiyo hali yote.** (Warumi 12:9; 1 Wathesalonike 5:22)

50) **Vitu visivyofaa kutajwa, ijapo vyafanyika kwa uchache, miongoni mwa watakatifu; uasherati, usinzi, uchafu, ulevi, tamaa mbaya, ghadhabu, ushindani, mapinduzi, chuki, mabishano, kujisifu, majiruno, wivu, mzaha, upumbavu na maongezi yasiyo mazuri.** (Waefeso 5:3-4; Wagalatia 5:19-21)

## KUHUSU MATENDO YAKO

51) **Mnapokula au kunywa au kufanya mambo yoyote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.** (1 Wakorintho 10:31; Wakolosai 3:17)

52) **Msiishi tena kwa wakati wenu uliosalia kutafuta mambo ya kujitosheleza kibinafi yatokanayo na tamaa asili, bali mkafanye mapenzi ya Mungu.** (1 Petro 4:2); **sadikini wenyewe kuwa wafu kwa dhambi lakini waliohai kwa utakatifu** (Warumi 6:11) **kuyatenda mapenzi ya Mungu kutoka moyoni** (Waefeso 6:6) **kwa wakati ujao, msiishi kwa nafsi zenu wenyewe, lakini kwa ajili yake yeye aliyewafia na kuamka tena.** (2 Wakorintho 5:15)

53) **Iweni wenye shauku kwa kazi njema, siku zote mkijazwa katika kazi ya Bwana, pasipo kuchoka kutenda mema.** (Tito 2:14; 1 Wakorintho 15:58; 1 Wathesalonike 4:1, Waebrania 6:11; Wagalatia 6:9, 2 Wathesalonike 3:13)

54) **Jihadharini na walimu wa uongo.** (Matayo 7:15; Wafilipi 3:2; 1 Yohana 4:1)

55) **Jihadharini na tamaa, msiweke hazina yenu duniani; muwe tayari kwa kila kazi njema.** (Luka 12:15; Matayo 6:19; Tito 3:1; Waebrania 13:5)

56) **Mpeni yeyote awaombaye, kwa wale wanaohitaji, watembeleeni mayatima na wajane katika hali zao ngumu; na muwape kwa ukarimu na moyo wenye furaha, mkikumbuka kuwa Bwana anampenda atoaye kwa moyo wa furaha, na anapendezwa sana na dhabihu za namna hiyo.** (Matayo 5:42; Warumi 12:13; 2 Wakorintho 9:6-8; Waebrania 13:16; Yakubo 1:27)

57) **Msijionyeshe mnapoyatenda mema ili mtambuliwe; usiruhusu mkono wako wa kushoto ujue kile ukitendacho mkono kwa wako wa kuume.** (Matayo 6:1-4)

58) **Msifanye kazi kwa madhumuni ya kuwa tajiri; msiwe na bidii ya kuwa na mali katika maisha ya sasa, mkiwa na chakula na mavazi, Tosheka**. (1 Timotheo 6:8; Yohana 6:27; Matayo 6:19)

59) **Utajiri ni inapokuja, ujapo kwa mkono wako, velekeze kwa ulinzi na kwa marafiki kwa kuutumia kwa ukarimu katika huduma ya Bwana, ambayo watumishi wake ni sisi.** (1Timotheo 6:10,17-19; Luka 12:18-21; 16:9-13; 1 Petro 4:10)

60) **Tembea katika Roho. Elekeza Maisha yako ili umuheshimu Kristo; Epukana na mwenendo wako mwovu wa kale; Jivike utu upya utokanao na ufahamu wa sura Takatifu.** (Wagalatia 5:16-26, Waefeso 4:24, 5:8-19, Wakolosai 3:9)

61) **Jitakaseni kutokana na nia mbaya za mwili na mawazo. Miili yenu ni viungo vya Kristo, na makao ya Mungu. Yeyote achafuaye hekalu la Mungu ataharibiwa. (**2 Wakorintho 7:1, 1 Wathesalonike 4:3, 1 Wakorintho 3:16-17, 6:15-20) **Msifungiwe nira moja na wasio amini au kushirikiana nao.** (2 Wakorointho 6:14)

62) **Jaribuni muwezavyo kuishi kwa amani na kila mtu.** (Warumi 14:19, 2 Wakorintho 13:11, Waefeso 4:3, Wakolosai 3:15, 1 Wathesalonike 5:13; 1 Timotheo 2:1,2; 1 Petro 3:11; 2 Petro 3:14)

63) **Hebu kila mmoja amhimize jirani yake katika maendeleo ya kiroho kama vile Paulo alivyowapendeza watu wote katika mambo yote, Akitafuta faida isiyo kwake mwenyewe, bali ya wengi ili waweze kuokolewa.** (Warumi 15:2, 1 Wakorintho 10:33)

64) **Fanyeni mambo yote pasipo manun'guniko wala ubishi.** (Wafilipi 2:14)

65) **Msisingizie au kunena maovu juu ya yeyote; Epukeni ugomvi na ushindani, Iweni wapole na wenye kusa wazisha amani kwa kila mmoja.** (Tito 3:2)

66) **Iweni wepesi wa kusikia, wasio wepesi kunena na wasio wepesi kukasirika.** (Yakobo 1:19)

67) **Ondokeni katika maovu yote, pasiwe na mmoja wenu atakayeteseka kwa kuwa muuaji, mwizi au mtenda dhambi, Jizuieni Kupeleleza mambo ya wengine.** (2 Timotheo 2:19, 1 Petro 4:15, 1 Yohana 3:15)

68) **IKiwa kunaye atesekaye kwa ajili ya mapenzi ya Mungu, wakikabidhi Maisha yao kwake katika kutenda mema, wala hawarudishi maovu kwa maovu, bali wakifurahia kuwa wao ni washirika katika mateso ya Kristo.** (1 Petro 4:19, 1 Wathesalonike 5:15, 1 Petro 4:13)

69) **Mjiepusheni na tamaa za ujana wenu, bali mfuateni utakatifu, Imani, upendo, amani, pamoja na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi.** (1 Timotheo 6:11; 2 Timotheo 2:22)

70) **Wacheni neno la Kristo likae kwa wingi ndani yenu, Mkilitamani kwa moyo wote kama afanyavyo Mtoto Mdogo kwa maziwa ya mama yake; Tafakarini juu ya mambo haya, Jitoeni wenyewe kikamilifu kwa ajili ya hayo.** (Wakolosai 3:16, 1 Petro 2:2, 1 Timotheo 4:15)

71) **Lipeni madeni yenu; msidaiwe na mtu kitu chochote, Bali mpendane.** (Warumi 13:7-8)

72) **Iweni chini ya watawala: Watiini mahakimu: Tiini kila sheria na amri ya mwanadamu, Isipokuwa pale ambapo inapingana na Sheria ya Kristo**. (Tito 3:1, 1 Petro 2:13-17, Warumi 13:6, Matendo 4:19)

## KUHUSU MAWAZO YAKO NA MATAMSHI

73) **Kuendelea kuyawazia maovu ambayo yanasisimua tamaa mbaya kunahesabiwa kiroho kama tendo la hatia. Inakanywa.** (Matayo 5:27-28)

74) **Angamiza maelekezi yako ya kiasili.** (Wakolosai 3:5; Wagalatia 5:24; 1 Wakorintho 9:27)

75) **Ondoeni visababishi vyote vya utelezi wa kiroho, au vizuizi kutoka kwa njia yako, hata Ikiwa kwa tahadhari ya uchungu na hasara.** (Matayo 5:29, Waebrania 12:1)

76) **Maneno yenu yawe na rehema siku zote, yakikolea munyu [Yenye kupendeza kiroho na wala si yasiyokolea]; msiruhusu mawasiliano machafu yatoke vinywani mwenu, bali maneno ya Busara, Iweni wenye kumaanisha kwa maadili, vnyofu na kuwa bila madoido.** (Matayo 5:37, Waefeso 4:29, Wakolosai 3:8, 4:6; Tito 2:7-8)

77) **Ikiwa kuna yeyote anenaye, wacheni anene kama msemaji wa Mungu.** (1 Petro 4:11)

78) **Semeni ukweli kila mmoja na Jirani yake; msidanganyane.** (Waefeso 4:25; Wakolosai 3:9)

79) **Msiape kamwe; Mnachohitajika ni kusema “Ndio” ikiwa unamaanisha ndio, “La” Ikiwa unamaanisha la”.** (Matayo 5:34; Yakabo 5:12)

80) **Kutoka kinywa kile kile hazifai kutoka baraka na laana.** (Yakobo 3:10)

## KUHUSU UHUSIANO WA NDOA

81) **Una uhuru wa kuoa umtakaye, lakini katika Bwana.** (1 Wakorintho 7:39) **ukitambua kuwa ndoa ni ya maisha** (Matayo 19:6; Warumi 7:1-2) **na Inafaa ionyeshe mfano wa fungamano la upendo kati ya Kristo na Eklesia.** (Waefeso 5:22-32)

82) **Waume na wake wasitengane isipokuwa kwa uasherati** (Matayo 19: 6-9; 1 Wakorintho 7:10) **ambao utawatenga kuingia katika Ufalme wa Mungu.** (1 Wakorintho 6:9)

83) **Mume au mke anapokuwa muumini pasipo mwenzake, asiachane naye, Iwapo mwenzake ataridhia kuishi naye kwa amani**. (1 Wakorintho 7:12-15)

84) **Waume wawapende, wawaheshimu, wawathamini na wawape wake zao utunzi bora wenye upendo.** (Waefeso 5:25; Wakolosai 3:19; 1 Petro 3:7)

85) **Wake wawapende, Wawatii, na wawe wasikivu kwa waume zao ambao ni vichwa.** (Waefeso 5:23-24; Wakolosai 3:18; 1 Petro 3:1)

## KUHUSU WAZAZI NA WATOTO

86) **Wazazi wawalee Watoto wao katika maelekezi ya ukweli, wakikumbuka kuwa Kristo ana nafasi ya kipekee kwa Watoto, na wawaelekeze katika mwenendo bora wa nidhamu.** (Waefeso 6:4, Wakolosai 3:21, Matayo 19:14; 1 Timotheo 3:4-5)

87) **Watoto wawatii wazazi wao kwa mambo yote.** (Waefeso 6:1, Wakolosai 3:20)

## KUHUSU MWENENDO KAZINI

88) **Waajiri wawe wakarimu, watenda haki na wenye huruma.** (Waefeso 6:9, Wakolosai 4:1)

89) **Waajiriwa wawe wenye bidii waaminifu pasipo na nia ya kuwafurahisha wanadamu, bali wawe waaminifu kana kwamba Wanamfanyia Kristo, hata kama waajiri wao watatokea kuwa wabaya.** (Waefeso 6:5-8; Wakolosai 3:22, 1 Timotheo 6:1-2; 1 Petro 2:18) **Waajiriwa wana uhuru wa kuacha kazi na kuondoka.** (1 Wakorintho 7:21)

90) **Ikiwa mwajiri ni ndugu, na mwajiriwa (Pia ni ndugu au dada), badala ya kutumia nafasi hii kutenda kinyume, wanafaa wawe wa manufaa na kutenda mema yawapasayo,** (1 Timotheo 6:2) **Mwajiri vile vile awe mwenye kusamehe hata akipata hasara.** (Filemoni 11-15)

## KUHUSU KUTOTII

91) **Ikiwa mfuasi mmoja hatii sheria ya mitume, ndugu wasiwe na uhusiano wowote na yeye.** (2 Wathesalonike 3:14) **Madai ambayo**

**hayajathibitishwa juu ya ndugu au dada hayafai kusikilizwa.** (Matayo 18:15-18, 1 Timotheo 5:19)

92) **Epukana na wale waletao migawanyiko**. (Warumi 16:17)

93) **Jitenge na kila atembeaye isivyostahili, au asiyeenenda kulingana na maagizo ya mitume.** (2 Wathesalonike 3:6,14). **Ondoa watu waovu miongoni mwa wafuasi wenu.** (1 Wakorintho 5:9-13)

94) **Dhambi ya wazi ikemewe mbele ya wote.** (Wagalatia 2:11-14; 1 Timotheo 5:20)

95) **Kataa au usikubali wawe katika ushirika wale ambao, baada ya kuonywa kikamilifu, wanakataa kuyakubali mafundisho au sheria za Bwana Yesu.** (Matayo 18:17; 2 Yohana msitari wa 8-10; 1 Timotheo 6:3-5, Tito 3:10)

96) **Ikiwa yeyote anakataa kufanya kazi mtu huyo asipewe msaada.** (2 Wathesalonike 3:10; 1 Timotheo 5:8)

## KUHUSU KUSANYIKO LA NDUGU NA DADA

97) **Mambo yote yafanywe kwa utaratibu na kwa mpangilio.** (1 Wakorintho 14:40)

98) **Mambo yote yafanywe kwa upendo, na kwa maelewano katika kutii.** (1 Wakorintho 16:14:1 Petro 5:5)

99) **Ndugu wanene kulingana na neno**, (1 Petro 4:11) **Waombe kwa ufahamu,** (1 Wakorintho 14:15) **wasifunike vichwa vyao katika Ibada au ushuhuda,** (1 Wakorintho 11:7) **wasiwe na nywele ndefu.** (1 Wakorintho 11:14) **Dada wakae kimya kwenye Eklesia** (1 Wakorintho 14:34; 1 Timotheo 2:11-12), **wavae mavazi ya adabu na busara**, (1 Timotheo 2:9; 1 Petro 3:3-4) **wafunike vichwa vyao katika kusanyiko.** (1 Wakorintho 11:3-10)

100) **Ndugu na dada wana uhuru katika maswala ya kula na kunywa, karamu, sabato, na siku kuu** (Wakolosai 2:16; 1 Wakorintho 10:25; Warumi 14 5:7), **ila wawe makini wasije wakawakwaza wenzao,** (Warumi 14:21; 1 Wakorintho 8:9; 10:32) **na hawana uhuru wa kufanya lolote lisilolingana na utakatiifu, au kwa utukufu wa Mungu.** (1 Wakorintho 10:31; 1 Petro 1:15-16; Waebrania 12:14)